# WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

JARIDA LA MTANDAONI | SEPTEMBA 2022





Afrika Inapaswa Kuwekeza katika Elimu kwa Wanawake....
**Uk. 01**



Ongezeni Nguvu ya Kuwezesha Wananchi Kiuchumi
**Uk. 09**



Uondoaji wa Kodi na Utoaji wa Ruzuku Umeleta Nafuu katika Soko
**Uk. 13**




# Afrika Inapaswa Kuwekeza Katika Elimu kwa Wanawake na Vijana kwa Maendeleo Endelevu ya Kijamii na Kiuchumi

Rais Samia Suluhu Hassan amesema nchi za Afrika zinapaswa kuwekeza katika rasilimali watu hususan elimu kwa vijana ili kuwa na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Sambamba na hayo, amesema maendeleo ya bara la Afrika yatapatikana haraka iwapo wanawake na vijana watawezeshwa kwa mitaji na taasisi za fedha pamoja na kuwaondolea vikwazo vya kibiashara hasa katika maeneo ya mipakani.

Rais ameyasema hayo Septemba 12, 2022 wakati akifungua Mkutano wa siku tatu wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam.

Mkutano huo wenye kaulimbiu "Wanawake na Vijana: Injini ya Biashara ya AfCFTA Barani Afrika" ni wa kwanza kufanyika tangu kuanzishwa kwa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika.

Alisema Afrika inahitaji nguvu kazi imara katika maendeleo ya kiuchumi hivyo uwekezaji katika elimu kwa vijana ni muhimu kwa kuwa sababu kubwa ya nchi nyingi zilizopiga hatua kimaendeleo ziliwaendeleza vijana kielimu.

Rais Samia alitoa mfano wa China ambayo alisema maendeleo yake yanachangiwa na kuwa na vijana wenye ujuzi hasa katika sayansi na teknolojia, hivyo nchi za Afrika hazina budi kuwekeza kwa vijana katika elimu ikiwamo ubinifu katika nyanja mbalimbali.

"China ni nchi ambayo inapigiwa mfano kwa maendeleo na siri kubwa ni uwekezaji iliyofanya ka vijana. Kampuni nyingi zinazofanya vizuri zinaongozwa na vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35 pamoja na matumizi ya sayansi na teknolojia Afrika inaweza pia kujenga uchumi imara kwa kuwekeza zaidi kwa vijana katika elimu hasa sayansi. Kwa kufanya hivi tutapiga hatua kubwa kiuchumi,"alisema.


KUSH
NMB
KARIBU TUKUHU
NMB


ERTY
5 GENDER EQUALITY
5 GENDER EQUALITY


WOMEN AND YOUTH IN TRADE
ASIA ACCESSORIES
SABUNI YA MDALASINI
SABUNI YA MDALASINI
SABUNI YA MANJANO
FRESH HANDMADE COSMETICS
SABUNI YA MWANI



# Ushirikishwaji Wanawake na Vijana ni Kichocheo cha Biashara




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman amesema ushirikishwaji wa wanawake na vijana katika ngazi mbalimbali ikiwemo nafasi za uwakilishi ni hatua moja wapo muhimu itakayochochea ufanisi katika biashara zinazoendeshwa na kundi hilo barani Afrika.

Ameyasema hayo Septemba 14, 2022 jijini Dar es Salaam kwa niaba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt.Hussein Ali Mwinyi wakati akifunga Mkutano wa Wanawake na Vijana katika Biashara chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika ulioanza Septemba12 hadi 14, 2022.

Kauli mbiu ya mkutano huu ilikuwa ni Wanawake na Vijana: Injini ya Biashara chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Hii ni kauli mbiu nzuri kabisa na ninaomba kuwashukuru na kuwapongeza wote walioshiriki katika kuibuni na kuipendekeza,"amesema.

"Nina imani kwamba, katika siku zote tatu mlizokuwepo hapa, mtakuwa mmeanza kuitekeleza kauli mbiu hii bila ya shaka. Hii ni kauli mbiu inayoishi na kama tukiendelea kuitekeleza kwa vitendo tutaona wanawake na vijana wengi zaidi wakishiriki na kunufaika katika biashara na hivyo kupelekea uchumi wetu kuzidi kukua na kuimarika, ikiwa ni pamoja na ajira.

**"Wito wangu kwetu sote ni kwamba tuendelee kuitekeleza kauli mbiu hii kwa vitendo hata baada ya mkutano huu, kwani ni dira muhimu sana kwa wanawake na vijana wetu kote barani Afrika,"amesema Mheshimiwa Othman kwa niaba ya Rais Dkt.Mwinyi.**

Pia amesema,anatarajia maazimio yote yaliyofikiwa katika mijadala ni msingi na chachu ya ushiriki wa wanawake na vijana wengi zaidi katika shughuli mbalimbali za biashara barani Afrika na duniani kwa ujumla na yatafanyiwa kazi na Sekretarieti ya AfCFTA kwa kushirikiana na nchi wanachama.

"Itifaki hii inatarajiwa kusaidia kuimarisha uwezo wa wanawake na vijana katika kutumia fursa zinazotokana na Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika. Kwa hivyo, natumia nafasi hii kuwaomba wanawake na vijana wa Afrika kuhakikisha kwamba mnatumia vyema fursa zinazopatikana katika Bara la Afrika na kwa manufaa ya nchi zetu za Afrika kwa kuzingatia utajiri tulio nao,"amesema.

Makamu wa Rais wa Kwanza alitumia nafasi hiyo kuzipongeza na kuzishukuru nchi zote za Afrika kupitia Sekreterieti ya Eneo Huru la Biashara la Afrika, kwa heshima kubwa waliyoipatia Tanzania.









# Itifaki ya AFCFTA ya Wanawake na Vijana Itaondoa Vikwazo Wanavyokabiliana navyo Kibiashara

Katibu Mkuu Mtendaji wa Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), Wamukele Mene amesema kuwa, mkutano wa wanawake na vijana katika biashara ni muhimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya vikao vya wakuu wa nchi na Serikali ya Umoja wa Afrika ambao waliazimia kupanua ushirikishwaji katika uendeshaji wa AfCFTA kupitia afua zinazosaidia vijana wa Afrika, wanawake na biashara ndogo na za kati (SMEs).

Mene ameyasema hayo wakati wa sherehe za ufunguzi wa Mkutano wa Wanawake na Vijana katika Biashara chini ya AFCFTA uliofunguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan Septemba 12, 2022 jijini Dar es salaam.

Amesema, sambamba na maagizo ya viongozi wa Afrika, Sekretarieti ya AfCFTA inafanya kazi ya maandalizi kuelekea katika hatua za kufanikisha Itifaki ya AfCFTA ya Wanawake na Vijana katika Biashara kuwaunganisha wafanyabiashara wasio rasmi wa mipakani katika uchumi rasmi kwa kutekeleza utaratibu wa biashara uliorasimishwa.

Mene amesema, itifaki hiyo inatarajiwa kushughulikia vikwazo ambavyo wanawake hukabiliana navyo wakati wa kufanya biashara barani Afrika.

Pia amesema, itaunda mazingira ambayo yataruhusu wanawake kutumia AfCFTA kupata masoko mengi, kuboresha ushindani wao, na kushiriki katika minyororo ya thamani ya kikanda.



# Wanawake na Vijana ni injini ya Biashara Afrika




Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt.Ashatu Kijaji amesema ni muhimu kuwawezesha wanawake na vijana katika biashara ili waweze kutumia fursa zilizopo katika Eneo huru la Biashara Barani Afrika AfCFTA .

Amesema kuwa,Tanzania na Bara la Afrika wakiwekeza zaidi katika sayansi na teknolojia kwa vijana wanaweza kuwa sehemu muhimu ya kustawisha uchumi kama ilivyo kwa Taifa la China.

Dkt Kijaji ameyasema hayo alipokuwa akimkaribisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan wakati wa sherehe fupi za ufunguzi wa Mkutano wa Wanawake na Vijana katika Biashara chini ya AFCFTA Septemba 12, 2022 jijini Dar es salaam .

"Ni imani yetu kwamba, wote tutatumia nafasi hii vizuri, kwa kuibua mijadala mipana itakayoleta tija kwa maendeleo ya Afrika yetu, hasa tukilenga kuwajengea uwezo wa kibiashara wanawake na vijana kwa kutoa mapendekezo ambayo yatazingatiwa katika maandalizi ya Itifaki ya wanawake na vijana katika biashara ambayo inalenga la kutatua changamoto za ushiriki wa wanawake na vijana katika biashara barani Afrika na hata dunia kwa ukubwa wake,"amesema Waziri Dkt.Kijaji.

Awali Mheshimiwa Waziri Dkt.Kijaji amesema,mkutano huo utajadili mada mbalimbali muhimu ikiwemo changamoto wanazokumbana nazo Wanawake na Vijana katika biashara za Mpakani (Reflecting on Challenges Women and Youth face in Cross Border Trade in Africa).

Pili ni namna ya kusaidia wanawake na vijana ambao ni kichocheo katika Sekta ya Ubunifu Barani Afrika (Supporting Women and Youth as Drivers of the Creative Industry in Africa).

Mada ya tatu ni juu ya namna ya kutumia nyenzo za kidigitali za biashara ili kuimarisha ushindani wanawake na vijana katika Soko la Eneo Huru la Afrika la Biashara (Leveraging Digital Solutions to Trade to Enhance Women's and Youth's Competitiveness in the AfCFTA Market).

Nne, ni namna ya kusaidia urasimishaji wa biashara za wanawake na wijana ili waweze kunufaika zaidi na Mkataba wa Eneo Huru (Women and Youth in Informal Cross Border Trade: Supporting the formalization of women and youth in trade for greater benefits under the AfCFTA).

Tano, ni majadiliano kuhusu Itifaki ya Wanawake na Vijana katika Biashara chini ya Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (Youth Roundtable on the AfCFTA Protocol on Women and Youth in Trade).

Sambamba na kuimarisha ushirikishwaji wa Wanawake na Vijana katika masuala ya kifedha (Promoting Financial Inclusion for Women and Youth in Trade).Katavi.






# Serikali Kuwawezesha Wajasiriamali na Wafanyabiashara Kiuchumi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesema itahakikisha bajeti inayotengwa na kuelekezwa katika Halmashauri kuwawezesha Wafanyabiashara na Wajasrimali inawafikia moja kwa moja ili ikawasaidia kuinua kiuchumi na kuchangia pato la Taifa kuongezeka.

Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhandisi Zena Ahmed Said ikiwa ni mwendelezo wa siku ya pili ya Kongamano la Wanawake na Vijana katika biashara chini ya Eneo huru la Biashara Afrika linalofanyika kuanzia Swptemba 12 hadi 14 , 2022 JNICC Dar es Salaam.

Vilevile amesema kwa Upande wa Zanzibar tayari zimetengwa fedha na kuwekwa katika benki ya CRDB ambayo inamuwezesha mwananchi kuchukua Mkopo pasipokuwa na riba wala kuweka dhamana kwani hapo awali wengi walikuwa wanakosa mikopo hiyo kwa kushindwa kupata vigezo hivyo vya dhamana

"Serikali ya Zanzibari iliona adha ya wananchi wake kukosa mikopo hivyo Serikali imepunguza ule mzigo uliokuwepo wa riba kubwa na kuweka dhamana ili mtu apate mkopo na sasa kila mtu ananufaika na fursa hiyo uaminifu wa kirudisha na wengine wapate.

Sanjari na hayo amesema kwa Tanzania bara kulikuwepo na sheria mahusi na inayoziielekeza halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 Ili wananchi wakope wakajiendeleze katika shughuli zao za kiuchumi.

Aidha amesema kongamano hilo limekuwa chachu ya kubadilishana uzoefu, kujenga uhusiano wa kibiashara na kutatua changamoto za biashara hasa maeneo ya mipakani wanazokumbana nazo Wafanyabiashara .

# Ongezeni Nguvu ya Kuwezesha Wananchi Kiuchumi




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amewataka wadau wote wa uwezeshaji wananchi kiuchumi waongeze nguvu katika kutoa huduma za uwezeshaji hasa maeneo ya pembezoni ya miji na vijijini ili kufikia malengo ya nchi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Ametoa wito huo Septemba 19, 2022 wakati akifungua kongamano la sita la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, lililofanyika katika ukumbi wa PSSSF, Jijini Dodoma.

"Pamoja na wito huo, Mikoa ambayo imeanzisha vituo vya uwezeshaji iendelee kuboresha miundombinu ili vituo hivyo vikidhi ubora na viwango katika kutoa huduma za uwezeshaji"

Amesema kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani Serikali imeendeleza azma yake ya kuwawezesha wananchi ambapo katika mwaka 2021/22, Serikali kupitia mifuko na programu mbalimbali Imeweza kutoa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 903 kwa wanufaika wapatao milioni 5.9 nchi nzima".

Ameongeza kuwa katika mwaka 2021/2022 jumla ya watanzania 72,395 walipata ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kutokana na ushiriki wao kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji (Local Content). "Aidha, miradi ya kimkakati ilitoa kandarasi ndogo kwa kuingia mikataba na kampuni 2,019 za Watanzania kwa huduma mbalimbali."


Mahali: Ukumbi wa LAPF - Dodoma


Mahali: Ukumbi wa LAPF - Dodoma
Tarehe: 19/09/2022
Kauli Mbiu: “Uwezeshaji Wananchi Katika Uwekezaji”

# Serikali Itaendelea Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kijaji amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imeendelea kuweka na kuimarisha miundombinu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Ameyasema hayo Septemba 19, 2022 wakati wa ufunguzi wa akifungua Kongamano la Sita la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, lililofanyika katika ukumbi wa PSSSF, Jijini Dodoma.

Ameongeza kuwa kupitia ruzuku zinazotolewa na Serikali wananchi wanapaswa kuona namna ya kuwekeza ili baadae waweze kuwasaidia Watanzania wengine kupitia faida aliyoipata. " Tuzitumie ruzuku hizi ili kuhakikisha tunalivusha Taifa letu na kuondokana na umasikini."

Kwa upande wake, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Beng'i Issa amesema kuwa baraza hilo limefanikiwa kuanzisha vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi 18 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Geita, Rukwa na Kigoma.

**"Vituo hivi kwa mwaka wa fedha 2021/22 vimeweza kuhudumia Watanzania 11,799, ambapo wanawakewalikuwa 6,157 (52%) na wanaume 5,642 (48%) na jumla ya mikopo ya shilingi bilioni 28 imetolewa katika vituo hivyo ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 kutoka kwenye mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2020/2021 na jumla ya biashara 15,860 zimeweza kurasimishwa katika vituo hivi, hii ni utekelezaji wa maelekezo uliyotoa mwaka 2018."**



# Uondoaji wa Kodi na Utoaji wa Ruzuku Umeleta Nafuu katika Soko



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt.Ashatu Kijaji amesema hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan za kuondoa baadhi ya kodi na kutoa ruzuku kwenye mafuta ya petroli na dizeli imeleta nafuu kubwa kwenye bei za bidhaa sokoni.

Dkt.Kijaji ameyasema hayo Septemba 15, 2022 wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu taarifa ya tathimini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini katika kipindi cha Agosti 15 hadi Septemba 15, 2022.
"Hata hivyo, kuanzia mwanzoni mwa mwezi Septemba hali ya upatikanaji wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye soko la dunia imeendelea kuimarika ambapo bei za bidhaa hizo zimeshuka na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji na usambazaji wa bidhaa. Kutokana na hali hiyo, tunatarajia katika siku zijazo bei za bidhaa nchini zitaendelea kushuka na kuleta unafuu katika soko la ndani,"amefafanua Dkt.Kijaji.

Akiendelea kutoa taarifa ya tathimini, iliyofanywa katika kipindi cha mwezi Agosti 15 hadi Septemba 15, 2022, Dkt amebainisha ongezeko dogo la bei katika baadhi ya bidhaa za vyakula hususani mchele, mahindi, na maharage ambalo limetokana na uhaba wa mvua kwenye maeneo mengi katika msimu wa kilimo wa mwaka 2021/2022 uliosababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao hayo.
.

Aidha Waziri Kijaji amesema Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inashirikiana na Tume ya Ushindani (FCC) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kufuatilia na kufanya tathmini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu nchini ikiwa ni mwendelezo wa utaratibu wa kutoa taarifa za kila mwezi za mwenendo wa bei nchini.

**Kuondoa baadhi ya kodi na kutoa ruzuku kwenye mafuta ya petroli na dizeli imeleta nafuu kubwa kwenye bei za bidhaa sokoni.**

# Serikali Itaendelea Kutatua Changamoto Bila Kufunga Viwanda

Waziri wa Uwekezaji,Viwanda na Biashara Dkt.Ashatu Kijaji amewataka wafanyakazi wa Kiwanda cha nguo cha 21th Century kilichopo mkoani Morogoro kuendelea kufanya kazi masaa 24 kwa siku saba kwa kuwa Serikali inaendelea kutatua changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kiwanda hicho bila kupunguza wafanyakazi au kufunga kiwanda.

Waziri Kijaji ameyasema hayo baada ya kufanya ziara katika kiwanda hicho Septemba 17, 2022 ambapo amesema kuwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi - CCM ya mwaka 2020/220 imeitaka Serikali kuendeleza viwanda vilivyopo na kufufua vilivyokufa ili kuweza kutengeneza ajira za watanzania milioni saba hivyo Serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan haipo tayari kuona kiwanda hicho kinafungwa.

Dkt.Kijaji pia amesema Serikali tayari kushirikiana na kiwanda hicho kutatua changamoto mbalimbali zilizowasilishwa zikiwemo kukatika katika kwa nishati ya Umeme, Maji pamoja na kuchukua hatua kwa wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa za nguo kinyemela nchini bila kulipa kodi na kuleta ushindani wa kibiashara baina yao na viwanda vya nguo nchini ikiwemo Kiwanda cha 21th century texile.

Aidha, ametoa ushauri kwa viongozi wa kiwanda hicho kuacha tabia ya kulalamika juu ya upungufu wa maji isikuwa wajaribu kutumia njia ya (recycling) ya kutumia maji yaliyopo na sio kuyaacha yakipotea bila sababu ya msingi na kuzingatia ubora wa bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo ili kuweza kuendana na ushindani wa soko la kimataifa.



# Watanzania Shirikianeni na Wawekezaji wa Nje ili Kupata Teknolojia




Watanzania Shirikianeni na Wawekezaji wa nje ili kipata teknolojia ya kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazoagizwa nje

Wawekezaji kutoka nchi za Afrika wametakiwa kuja kuwekeza nchini Tanzania na kuzalisha bidhaa mbalimbali ili kuongeza uchumi wa viwanda ambao ndiyo sera na msingi katika Serikali ya Awamu ya sita iliyo chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe, wakati akizungumza na waandishi wa habari Septemba 22, 2022 katika uzinduzi wa maonyesho ya Kimataifa ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Diamond jubilee Jijini Dar es Salaam.

Aidha, Kigahe amewaomba wafanyabishara hao kutoka nje wa shirikiane na watanzania katika kuleta teknolojia kupitia elimu lakini pia bidhaa ambazo ni muhimu sana kwenye maeneo tofauti tofauti hasa kwenye sekta ya Kilimo kwa kiwa Tanzania ni wazalishaji wa mazao mengi yakiwemo ya chakula na biashara na yanauzwa nje kama malighafi na yakiwa hayajaongezwa thamani na hivyo kupoteza ajira nyingi.

**"Tunaweza kuona teknolojia nyingi za kisasa ambazo tunaamini na sisi watanzania tukiwa katika mpango wetu wa kuwa na uchumi wa viwanda lazima tuwe nazo hivyo tunawaomba waonyeshaji hawa kutoka nchi mbalimbali kuja kuwekeza katika nchi yetu , kuzalisha bidhaa mbalimbali ambazo sisi kama Tanzania tunatumia fedha nyingi kuziagiza nje kwaajili ya matumizi yetu ya ndani."**

Naibu Waziri Kigahe amesema ni muda muafaka sasa teknolojia hizo ziwasaidie na watanzania kuzalisha bidhaa zinazotokana na kilimo, chakula na biashara zinazozalishwa hapa Tanzania. Jivyo amehamasisha kupata teknolojia za kisasa ambazo hazina athari kwenye mazingira ambazo zitaendana na hali halisi ili kupunguza fedha nyingi zinazokwenda nje.

"Wekezeni pia katika sekta ya usafiri. Tumeona wenzentu wanatengeneza pikipiki zinzotumia umeme, hizi zitasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira lakini pia kupunguza gharama za kuagiza mafuta na upotevu wa fedha za kigeni na kuongeza ajira nchini na zitaongeza kasi ya maendeleo yetu kwasababu bidhaa nyingi zitaongeza thamani nyingi". Amesema Kigahe.

Kuhusu vifungashio, Kigahe amesema, moja ya changamoto ambazo zipo katika uzalishaji wa bidhaa Tanzania ni vifungashio vilivyobora ambapo kwa baadhi ya makampuni ambayo yanazalisha vifungashio kutoka India ambao wangekuja kuwekeza nchini Tanzania wangeweza kusaidia kuongeza nguvu ya uzalishaji wa vifungashio bora na vilivyo na bei nafuu na kupunguza uagizaji wa vifungashio kutoka nje vinavyoongeza gharama ya mlaji.

Kigahe amesema kwa sasa vifungashio vingi kwa upande wa Afrika Mashariki vinaagizwa Kenya ila kwa nje vinaaagizwa kutoka china na India.







# Kagueni Mizani Kuepusha Migogoro

Naibu waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe (Mb) amewataka wakala wa Vipimo Mkoani Mtwara kukagua Mizani yote ambayo itatumika katika mauzo ya korosho kwa msimu huu unaoatarajia kuanza mwaka huu.

Mhe. Kigahe ametoa maagizo hayo tarehe 10 Septemba, 2022 alipotembelea na kufanya ukaguzi katika Ofisi ya Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Mtwara na kusema kuwa ukaguzi huo wa Mizani kufanyika mapema na mara kwa mara utasaidia wakulima pamoja na wafanyabiashara wote kunufaika na zao la korosho na kupunguza migogoro ya ujazo au Vipimo sahihi.



"Mtwara ndiyo kitovu cha biashara ya korosho na uchumi wa nchi hii Kama tunavyojua trillioni nyingi za fedha zinatokana na mauzo ya korosho Sasa tusingependa kuona Mtwara inakuwa nyuma kunufaika na zao hilo na moja ya njia ya kuhakikisha Mtwara inanufaika ni kuhakikisha mizani inakaguliwa mara kwa mara hasa msimu huu unaokuja wa mauzo ya korosho" Amesema, Mhe. Kigahe.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Ahmed Abbas Ahmed Amesema kuwa Mtwara ni kitovu Cha Biashara na uchumi wake unakuwa Kwa Kasi zaidi.

Mhe. Kanali Ahmed amesema kuwa serikali ya awamu ya sita imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo ikiwemo miradi ya miundombinu ya barabara, zahanati, shule pamoja na kuishughulikia ujenzi wa Viwanda vya kuchakata malighafi za Kilimo, Viwanda vya Saruji, Sabuni na sukari.

Mhe. Kanali Ahmed amesema kuwa WMA ina jukumu kubwa la kuhakikisha inakagua na kuisimamia Vipimo sahihi vya Mizani yote ya magari, mitungi ya gesi, dira za maji na mafuta.

Naye Kaimu Mtendaji Mkuu wa WMA Bw. Deogratius Maneno Amesema kuwa WMA ina jukumu kubwa la uhakiki wa Mizani, dira za maji na gesi, kutoa ushauri wa kitaalamu wa Vipimo na kufanya kaguzi za Mizani na Vipimo.

Mhe. Kigahe katika ziara yake Mkoani Mtwara ameambatana na Viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Hashil Abdallah na Mkuu wa Wilaya ya Mtwara mjini Mhe. Dunstan Kyobya




# Dkt. Kijaji: Toeni Maoni Sheria Mpya ya Uwekezaji

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) ametoa rai kwa watanzania kutoa maoni kuhusu marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji iliyowasilishwa bungeni hivi karibuni ili iweze kukamilika kikamilifu ikijumisha maoni ya wadau wote.

Dkt. Kijaji ameyasema hayo wakati wa ufunguzi rasmi wa Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Italia uliofanyika katika ukumbi Kimataifa wa Mwalimu Julias Nyerere Septemba 30, 2022.

Dkt. Kijaji pia ameainisha kuwa Sheria iliyokua ikitumika awali ilimtaka mwekezaji mtanzania kuwa na dola laki moja kama mtaji, ili kuweza kupata vivutio vinavyotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), lakini kulingana na marekebisho yaliyowasilishwa bungeni yameshusha takwa la kiwango cha dola laki moja hadi dola elfu hamisini ili kupata vivutio.

Aidha, Dkt. Kijaji, amesema Serikali ya Awamu ya sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, imendeleza mfumo wa uwekezaji wa Tanzania kwa kuweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara ili kukuza uwekezaji wa ndani na nje.

Ameeleza kuwa Serikali imefungua milango kwa kila mtu anayependa kuleta mtaji na kufanya biashara Tanzania kwani Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanania (TIC) inatoa aina mbalimbali za vivutio vya uwekezaji ikiwemo maeneo ya uwekezaji na wawekezaji wataweza kufikia soko la Afrika Masharaiki na Afrika kupitia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AFCFTA) ambapo Tanzania ni Mwanachama.



Kwa upande wake Balozi wa Italia nchini Tanzania, Mhe. Marco Lombardi amesema mazingira ya biashara nchini Tanzania yameboreshwa na yamelingana na standadi za mazingira ya makampuni ya Italia ambayo yamewekeza zaidi ya Dola bilioni mbili (2) Tanzania

Naye Balozi wa Tanzania nchini Italia Bw. Mahmoud Kombo amewahimiza watanzania kujitokeza kwa wingi na kuchangamkia fursa mbalimbali za biashara kati yao na wafanyabiashara wa Italia hususani katika kuendeleza sekta za kilimo kama mashine za kuchakata mazao na mashine za vifungashio.

Aidha, Rais wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture, (TCCIA) Bw. Paul Koyi amesema jukwa hilo limesaidia kupatikana kwa makubaliano ya pamoja kati ya chemba ya biashara ya Tanzania na Zanziba na Chemba ya Genova ya Italia ambayo yanatarajiwa kuleta mafanikio na faida baina ya Nchi hizo ili kukuza uchumi wa Taifa na kuongeza ajira kwa wananchi vijana na kina mama.



# Dkt. Mwigulu : Bei za Bidhaa Zitashuka



Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.) amesema mfumuko wa bei ulioshuhudiwa kwa siku za hivi karibuni na kusababisha baadhi ya bidhaa kupanda bei mara dufu huenda ukaanza kupungua kutokana na kushuka kwa nishati ya mafuta katika soko la dunia.


Waziri huyo ameeleza hayo alipokuwa akifungua Mkutano wa Kimataifa wa Taasisi ya Kuhakikisha Uendelevu wa uwekezaji Duniani (MIGA) inayofanya kazi chini ya Benki ya Dunia uliofanyika Septemba 14, 2022 jijini Dar es Salaam.

“Utakumbuka mafuta bei ziliku zinapanda sana lakini katil taarifa iliyotoka hivi maju mafuta yamepungua japo hay jafika tulipokuwa mwanz kabisa ila umeona punguzo zaidi ya Sh. 400 ambalo ni pu guzo kubwa” Mwigulu alisema

Alisema pia kwakuwa bei z mafuta zimeshuka na za usaf ishaji zitashuka tunakokwend bidhaa na zenyewe zitaitik nazo zitashuka” Mwigulu

**“Tunaamini kwa jitihada hizi za Rais za kuweka Bilioni 100 kila mwezi bei za mafuta zitaendelea kupungua, bei za mafuta zinapopungua mfumuko wa bei nao utapungua tunakoenda, bidhaa mnazoona hapa kati zimepanda ziliitikia kupanda kwa bei za mafuta.”**

Jarida la Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara | Agosti 2022



# Serikali Kuendelea Kuweka Mazingira Bora ya Uwekezaji

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Dkt Ashatu Kijaji ( Mb.) amesema Serikali imeonyesha dhamira ya kuboresha uwekezaji kupitia majadiliano na wawekezaji na kiwawezesha wawekezaji kifikia malengo yao nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari Septemba 15 wakati wa kuhitimisha mkutano wa siku mbili wa Wakala wa Uwekezaji wa Kimataifa (Miga) chini ya Benki ya Dunia (WB) na wawekezaji jijini Dar es salaam.

"Mahitaji ya uwekezaji ni makubwa, ndiyo maana mnaona tunaita mikutano kama hii ili tubadilishe mawazo kwa pamoja ya fursa tulizonazo na changamoto walizonazo wafanyabiashara wetu," Amesema Dkt. Kijaji.

Alisema mkutano huo umeshirikisha mataifa 10 na kampuni 75 za kimataifa lengo likiwa ni kushirikiana na kampuni za ndani katika uwekezaji.

"Sisi Serikali tunawahakikishia ushirikiano mkubwa kwa sababu tayari Rais Samia Suluhu Hassan, amefungua nchi yetu katika diplomasia ya uchumi," Alisema.

Pia Waziri Kijaji alisema kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2022, Serikali imepunguza tozo zilizokuwa kero kwa wawekezaji na imeondoa tozo sumbufu zaidi ya 132 ili kuvutia wawekezaji kuja Tanzania.

Akizungumza kwa upande wa sekta binafsi, mtaalamu wa diplomasia ya uchumi kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Raphael Magamba amesema mkutano huo umeongeza hamasa ya wawekezaji wa kigeni kuja nchini na wamejadili changamoto na utatuzi wake.

"Kwa sekta binafsi ya Tanzania tumefaidika, kwanza nchi imefunguka na wawekezaji wamekuja na Serikali imewapa uhakika wa mitaji yao. Kama mtu alikuwa anawekeza dola 5 milioni, anaweza kuweka hadi dola 100 milioni bila kuwaza kwamba uwekezaji wake hapa Tanzania utakuja kupotea,"Alisema.

Alisema awali walikuwa na changamoto ya wawekezaji wa ndani kukosa mitaji, lakini kupitia mkutano huo wamehakikishiwa kuipata.

"Kupitia Benku ya Dunia kuna Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) linalotoea mikopo kwa wawekezaji na Miga ipo ambayo inatoa uakika wa uwekezaji, kwa hiyo tunafarijika kwa hilo," alisema.

# Wawekezaji Tumieni Teknolojia za Kisasa Kutunza Mazingira



Naibu Waziri wa Uwekezaji,Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe ameyashauri mashirika na kampuni za ndani na nje ya nchi yanayotaka kuwekeza nchini kuzingatia utunzaji wa mazingira kwa kutumia teknlojia za kisasa zitakazowezesha utunzaji wa mazingira ili kuvutia wawekezaji wengine zaidi.

Kigahe ameyasema hayo Septemba 27, 2022, jijini Dar es salaam wakati wa uzinduzi rasmi wa Mradi wa Kanda Maalum ya Kiuchumi ya Mkinga Mkoani Tanga unaotarajiwa kuzalisha ajira zaidi ya 3000 katika awamu ya kwanza.

Aidha, amewapongeza wawekezaji hao kwa kuziona fursa zilizopo mkoani Tanga na kisisitiza kuwa Serikali itawaunga mkono kwa kuwezesha uwekezaji huo kuwa na tija kwao na kwa Serikali kwa kuwa Sekta binafsi ni moja ya sehemu kubwa katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakua

"Serikali inatarajia uwekezaji huu kuwagusa moja kwa moja wananchi wa wilaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga na Taifa kwa ujumla kwani hiyo ndio itakuwa njia sahihi ya kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na hivo kuleta Tija katika uchumi wa Taifa" Amesema Kigahe

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Mkinga Special Economic Zone Bw. Ally Kassim amesema lengo la Mradi huo ni kutekeleza maagizo ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha uwekezaji nchini unaongezeka ili kuleta usawa wa kiuchumi katika maeneo yatakayofanyiwa uwekezaji husika.

Aidha, amesema Wawekezaji hao wamethibitisha kuwa hadi sasa jumla ya wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali ikiwemo Brazil, Misri, Tunisia, Bulgaria, GCC, Ufilipino na India wameonyesha nia ya kuwekeza katika mradi huo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Omary Mgumba amesema wawekezaji hao wamevutuwa na fursa mbalimbali ambazo ni Bandari, Bomba la mafuta pamoja na Ardhi yenye rutuba zinazowarahisishia kuapata malighafi na usafirishaji wa bidhaa na vitendea kazi kutoka ndani na nje ya nchi.



# Watanzania Changamkieni Fursa za Soko la Mazao ya Chakula Comoro

Naibu Waziri Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe amewataka wafanyabiashara wa Tanzania kuchangamkia fursa ya soko la mazao ya chakula nchini Comoro.

Mhe. Kigahe ameyasema hayo baada ya kikao chake na Balozi wa Comoro nchini Tanzania, Dkt. Ahmada El Badaoui pamoja na wafanyabiashara wa Tanzania na Comoro kilichofanyika mkoani Dodoma.

Aliwataka Watanzania kutumia fursa hiyo kwani nchi ya Comoro wanauhitaji wa chakula hasa mchele na nyama hivyo alitoa rai kwa wazalishaji na wafanyabiashara kuchangamkia fursa ipasavyo.

“Wamekuja kuona namna gani wanaweza kupata bidhaa mbalimbali, hususani mihogo, mchele, nyama, kuku, maziwa na saruji, pamoja na vifaa vya ujenzi.”

Mhe. Kigahe ameitaka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) na Wakala wa Vipimo (WMA) kuratibu vizuri matumizi ya fursa ya soko la Comoro ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa Wazalishaji, Wafanyabiashara na Wakulima wanafaidika na soko hilo.

Awali Mhe. Balozi wa Comoro nchini Tanzania, Mhe Dkt. Ahamada El Badaoui Mohamed, aliwahakikishia wafanyabiashara wa Tanzania uwepo wa soko la uhakika nchini Comoro.
“Tuna mahitaji ya bidhaa za chakula kama vile mihogo, mchele, nyama, maziwa na vifaa vya ujenzi.”Alisisitiza.

Balozi Dkt. Ahamada El Badaoui alianisha changamoto wanayokutana nayo kwa sasa ni bei kubwa ya bidhaa hizo. Hivyo ameiomba Serikali ya Tanzania

# Baraza Hakikisheni Malengo ya TIRDO na Taifa Yanafikiwa

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) ameliagiza Baraza la Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) kuandaa mkakati ya utekelezaji wa mipango ya Shirika ili kuhakikisha malengo ya Taifa, Wizara na TIRDO yanafanikiwa.

Kigahe ameyasema hayo katika hafla fupi ya uzinduzi wa Baraza hilo iliyofanyika Septemba 28, 2022 jijini Dar es Salaam ambapo Baraza hilo na Menejimenti litapimwa kwa kutumia mkataba wa utendaji kazi (Perfomance Contract) utakaosainiwa kati yao na Msajili wa Hazina.

Aidha, Kigahe ameliagiza Baraza hilo kutoa ushauri sahihi unaolenga kuleta tija kwa shirika nankutatua kutatua changamoto za shirika, kuleta mawazo mapya ya kuboresha uendeshaji wa shirika na utoaji wa huduma mpya zitakazoimarisha utendaji kazi na utatuaji wa migogoro wakati wa utekelezaji wa majukumu.

Kigahe amewaeleza wajumbe wa Baraza hilo kuwa watunza nidhamu wa Menejimenti na watumishi wa Shirika hilo kwa niaba ya Serikali ili kuhakikisha Menejimenti inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi.

"Nimeona vile vile, bunifu mbalimbali ambazo zimelenga kuleta suluhisho kwa Watanzania kwa kusaidia teknolojia rahisi za kuongeza thamani ya mazao na hivyo kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati," ameongeza Kigahe.

Vilevile, ametoa rai kwa Baraza hilo na Mejimenti, kuendelea kuandika maandiko mbalimbali (project proposals) kwenda kwa wadau mbalimbali wa kisekta ili kupata fedha za utafiti na kubuni teknolojia rahisi ambazo zitaendelea kuwasaidia wakulima, wavuvi, wafugaji na sekta zingine zote zinazotoa ajira kupitia viwanda.






Naibu Waziri wa Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe na Balozi wa Marekani Nchini Tanzania Mhe. Donalt Wright wamezindua rasmi ziara ya makampuni ya Kimarekani yatakayotembelea Tanzania kujionea Fursa za kibiashara na kiuwekezaji.

Makampuni 20 ya Kimarekani yatakayoshiriki ziara hiyo yanatoka katika sekta za biashara za kilimo, nishati, huduma za afya , TEHAMA na Viwanda





# Dkt. Kijaji: Wadau wa Sekta ya Nguo Ainisheni Changamoto Tuzishughulikie

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) amewashauri wadau wa sekta ya nguo kuainisha changamoto za kisera, kikodi na kiutendaji wanazokutana nazo ili azifanyie kazi.

Dkt. Kijaji ameyasema hayo Sepetemba 26, 2022 jijini Dodoma alipokutana na wadau wa sekta ya nguo na walio chini ya Chama cha Wazalishaji Nguo na Mavazi Tanzania (TEGAMAT) ili kujadili changamoto wanazokutana nazo.

Aidha, Waziri Kijaji amewashauri wadau hao kutokufunga viwanda, kwa kuwa ni sekta inayotoa ajira nyingi kwa vijana.

"Njoni tukae tuongee, tupange kwa.pamoja tuone cha kufanya, tunataka viwanda vifanye kazi katika Serikali ya Awamu ya Sita amnayo ni sikivu". Amesema Dkt. Kijaji.

Aidha ameongeza kuwa nia ya Serikali ni kuona viwanda nguo vya Tanzania vinakua shindani na vinahudumia Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Akiongea mbele ya Waziri Kijaji, Katibu Mtendaji wa TEGAMAT Bw. Adam Zuku ameomba kuwe na ushindani wa haki na usawa kati ya waingizaji vitenge na wazalishaji ili waweze kushindana katika soko la nje.

"Tunatamani kuhudumia soko la SADC,EAC, ACFTA" alisema Zuku.

Aidha, Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau hao wameiomba Serikali kuanzisha mitaala ya nguo kwa kuwa kwa sasa kuna uhaba wa wataalamu hao . Pia wameiomba tozo zinazotozwa na Taasisi mbalimbali za Serikali kujumuishwa kwa pamoja ili kuwapunguzia usumbufu na gharama kubwa za uendeshaji.



# Tanzania na Benki ya Dunia Kuendelea Kushirikiana Kuboresha Mazingira ya Biashara

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt.Ashatu Kijaji amesema Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (Blueprint) ili kuvutia uwekezaji na kuwezesha ufanyaji biashara wenye tija utaokuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

Dkt. Kijaji ameyasema hayo wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na
Mkurugenzi wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika anayeshughulikia Ukuzaji wa Uchumi na Taasisi kutoka Benki ya Dunia (WB), Dr.Asad Alam na ujumbe wake kuhusu fursa za uwekezaji na ufanyaji biashara zilizopo Tanzania. Mazungumzo hayo yamefanyika katika Ofisi za Wizara jijini Dodoma Septemba 29, 2022.

Akiwa ameambata na Viongozi wa Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara akiwemo Naibu Katibu Mkuu Dkt. Hashil Abdallah, Dkt. Kijaji amemhakikishia Mkurugenzi huyo kuwa Serikali iko tayari kushirikiana na Benki ya Dunia kuanzisha na kuendeleza programu mbalimbali za kuwawezesha wajasikiamaki wadogo na wa kati kuwekeza na kufanya biashara ili kukuza uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Aidha, Dkt. Kijaji amesema Serikali inaendelea kufanya mamoresho mbalimbali kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini ( Blueprint) ikiwemo kupitia na kurekebisha sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Uwekezaji pamoja na kupunguza tozo mbalimba ambazo zimekuwa kikwazo katika ufanyaji biashara na uwekwzaji.

Naye Mkurugenzi huyo wa Kikanda chini ya Benki ya Dunia amesema Programu hiyo ya kukuza uchumi na Taasisi amesema Benki dunia kupiyia programu hiyo iko tayali kuwawezesha wajasilimali watanzania katika sekta mbalimbali kuendeleza biashara zao zitakazoongeza ajira, pato la Taifa na kuleta maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi kwa ujumla.




Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Bw. Ally Gugu (wa katikati) akiwa na Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe. Misawa (wa kulia) wakati wa mazungumzo kuhusu kuimarisha mahusiano baina ya Tanzania na Japan pamoja na kujadiliana fursa za uwekezaji nchini kwenye Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mazungumzo yamefanyika katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania ( TIC ) Septemba 29, 2022.



# Wafanyabiashara Zingatieni Masharti ya Ubora wa Bidhaa zinazoingizwa Nchini

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara Wizara ya Uwekezaji,Viwanda na Biashara Bw.Christopher Mramba amewashauri wafanyabiashara kuzingatia sheria na kuendelea kujenga utamaduni wakuzingatia masharti ya ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa kuwa Serikali haitaacha soko la Tanzania liwe dampo la kuweka bidhaa zisizo na ubora.

Bwana Mramba amayasema hayo Akizungumza na waandishi wa habari Septemba 30 , 2022 katika ofisi za Shieika la Viwango Tanzania (TBS) Jijini Dar es Salaam wakati wa uchunguzi wa mabati yaliyoingizwa nchini na kampuni ya uagizaji na usambazaji wa mabati nchini URHOME Company Limited

"Tutaendelea kushirikiana na vyombo vya Serikali kufuatilia bidhaa ambazo zimeingia sokoni kinyume na sheria na kuchukua hatua stahiki za kisheria" Amesema Bw. Mramba.

Aidha, Bw. Mramba ametoa wito kwa wafanyabiashara wote nchini kuzingatia uaminifu na matumizi mazuri ya fursa zinazotolewa na Serikali za kuweka mazingira wezeshi ya biashara ikiwemo hii fursa ya kutoa kibali cha masharti maalumu ya kutoa mzigo bandarini ili bandari yetu iendelee kuwa na ufanisi unaotakiwa na pasiwe na msongamano ili biashara nyingine ziweze kufanyika.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Bw. David Ndibalema amewahimiza wafanyabiashara na waingizaji wa bidhaa kutumia vizuri vibali vya masharti kwa kuhakikisha wanazingatia yale masharti ambayo yamewekwa wakati wa kutoa vibali hivyonikiwemo kutokusambaza, kuuza, au kutumia njia yoyote ile kutoa mzigo kabla ya uchunguzi kukamilika.

Aidha, TBS imeiandikia barua kampuni hiyo ya uagizaji na usambazaji wa mabati nchini URHOME Company Limited kuhakikisha ndani ya siku tatu wawe wametoa taarifa ya mabati 2176 kati 125280 yapo wapi baada ya kufanyiwa ukaguzi na kugundulika hayajakidhi viwango.

Naye, Meneja wa uthibiti wa Shehena zinazoingia na kutoka nchini Mhandisi Saidi Mkwawa amesema Kampuni hiyo baada ya kuingiza nchini mabati hayo, TBS ilichukua sampuli na kuzipeleka kwenye maabara ya Shirika ili kubaini kama zimeweza kukidhi viwango stahiki kwa mujibu wa sheria .

Pamoja na hayo Mhandisi Mkwawa amesema watahakikisha mabati yote yanapatikana na zoezi la uteketezaji litaendelea sambamba na mengine.



# CAMARTEC na Maswa Kukubaliana Kuanzisha Kitovu cha Kuendeleza Zana za Kilimo

Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb) amepongeza juhudi kubwa zilizofanywa na Viongozi wa Wilaya ya Halmashauri ya Maswa kwa kushirikiana na Kituo cha zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) katika kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Kigahe ameyasema hayo Septemba 5, 2022 katika ukumbi wa Wizara uliopo mji wa Serikali Mtumba aliposhuhudia utiaji saini wa hati za makubaliano (MoU) baina ya CAMARTEC na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kuhusu uanzishwaji wa kitovu cha Teknolojia za kihandisi (Engineering Technol-

cha Mwandete Wilayani Maswa Mkoa wa Simiyu.

"Juhudi kubwa za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ni kuinua Sekta kilimo kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa ajili ya chakula na malighafi za viwanda vyetu, hivyo tutumie rasilimali za nchi kwa manufaa ya wananchi wetu katika kuwaletea maendeleo" Amesema Kigahe.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CAMARTEC Mhandisi Pythias Ntella ameleza kuwa wafanyabiashara wa Maswa walikuwa na changamoto ya ukaushaji

mvua ambao ulikiwa unachukua muda mrefu kutokana na ukosefu wa nishati ya jua hali inayosababisha Kiwanda kushindwa kukidhi mahitaji ya wateja na pia hasara kutokana na kupungua kwa ubora wa viazi.

Mhandisi Ntella amesema kuwa ujio wa Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (KITEKI) kitakuwa ni cha kwanza na cha aina yake nchini, ambapo kitatumika kama mfano (pilot) na kutoa uzoefu mkubwa kwa CAMARTEC utakaoiwezesha kuanzisha vitovu vya namna hiyo kwenye Kanda Saba nchini

katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Maswa Mhe. Aswege Kaminyoge amesema kuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara imefanya juhudi kubwa mara baada ya ziara ya kikazi ya Naibu Katibu Mkuu Mhe. Dkt. Hashil Abdallah Wilayani Maswa na kutembelea Kijiji cha Mwandete kilichopo Kata ya Sangamwalugesha Mkoani Simiyu.

"Madhumuni ya ziara ya Naibu Katibu Mkuu Mhe. Dkt. Hashil Abdallah yalikuwa ni kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa Uanzishwaji wa Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (Engineering Technology Hub-ETH) unaotarajiwa kuanzishwa kwenye Kijiji cha Mwandete, hivyo natoa shukrani za dhati kwa Viongozi wote waliofanya juhudi kubwa za uanzishwaji wa kituo hiki akiwemo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Mkurugenzi wa Halmashauri na waheshimiwa madiwani kwa kukubali kwa kauli moja". Amesema Mhe. Kaminyoge.

Akitoa neno la Shukrani Mbunge wa Maswa Mhe. Stanslaus Nyongo amesema kuwa uanzishwaji wa Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (KITEKI) katika Kijiji cha Mwandete unaenda kutatua changamoto nyingi wanazokumbana nazo wakulima ikiwemo kukosa teknolojia rais ya kukaushia mazao yao, ajira inaenda kuongezeka na kipato kwa wananchi.

Mhe. Nyongo amesema kuwa pongezi nyingi anazitoa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwani amewajali wananchi wa Maswa kwa kuwapelekea fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya Maendeleo.





# ITRACOM Fertilizer Kuanzisha Kiwanda cha Saruji Kigoma

Naibu Waziri Wizara ya Mikakati ya Serikali ya kuvutia wawekezaji imewezesha Kampuni ya ITRACOM FERTILIZERS ya Burundi kuwekeza kiwanda cha saruji mkoani Kigoma.

Hayo yamebainishwa bungeni Septemba 20, 2022 na Naibu Waziri, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe wakati wa kujibu swali la Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, Nashon Bidyanguze.

Katika swali lake, Bidyenguze alitaka kujua ni lini Serikali italeta mwekezaji wa kiwanda cha sementi katika Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Akijibu swali hilo, Kigahe amesema

Amesema Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ili kuhamasisha na kuvutia wawekezaji ikiwemo kwenye sekta ndogo ya saruji nchini.


Amesema Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kigoma kimeweza kuvutia Mwekezaji (ITRACOM FERTILIZERS CO. LTD) kujenga kiwanda cha saruji.

Kigahe amesema kuwa pia mwekezaji huyo amepewa ekari 47 za ardhi katika Eneo la Uwekezaji la Kigoma (KiSEZ) na kuwa

Wilaya ya Uvinza pia itanufaika na mwekezaji huyo.

Amesema Serikali inaendelea kuvutia wawekezaji zaidi ili kuwekeza katika mkoa wa Kigoma ikiwemo Wilaya ya Uvinza.







# Serikali Kupanua Wigo wa Biashara Baina ya Tanzania Bara na Zanzibar

Katika kuendelea kupanua wigo wa biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, Serikali imekuja na mipango na mikakati mbalimbali ikiwamo ya kufanya tathmini ya kubaini vizuizi visivyo vya kikosi.

Haya yamebainishwa na Naibu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe wakati wa kujibu swali la msingi la Mbunge wa Jimbo la Konde, Mohamed Said Issa (ACT-Wazalendo).

Katika swali lake Mhe. Issa alitaka kujua Mpango wa Serikali wa kuongeza wigo wa biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ili kuongeza mapato.

Akijibu swali hilo, Mhe. Kigahe anasema: "Wizara ina Mipango na Mikakati mbalimbali ili kuendelea kupanua wigo wa Biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar"

Anataja mipango na mikakati hiyo kuwa ni kuendelea kutoa elimu na kuongeza hamasa zaidi kwa makampuni ya Tanzania Bara na Zanzibar kushiriki katika Maonesho mbalimbali yanayofanyika ndani ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Amesema pia kufanya tathmini ya kubaini vizuizi visivyo vya kikodi (Non-Tariff Barriers) na kuzishirikisha Mamlaka mbalimbali ikiwemo Mamlaka za Mapato za Tanzania Bara (TRA) na Zanzibar (ZRA) kwenye majadiliano ya pamoja ili kupanua wigo wa Biashara.

" Upanuzi wa ushirikiano wa kibiashara unazingatia na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizopo."

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Viwanda, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt. Wilson Lugano mwenye suti akitazama chumvi katika kiwanda cha Neel salt kilichopo Mkuranga Pwani, wengine ni Mkurugenzi wa Kiwanda hicho Bw. Druvu Kumari mwenye Tshirt nyekundu. Dkt Lugano na timu ya wataalamu kutoka wizara ni walitembelea kiwanda hicho kwa lengo la kujionea utendaji kazi na kusikiliza changamoto za kiwanda hicho.





Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Viwanda Wizara Uwekezaji Viwanda na Biashara Dkt. Wilson Lugano (wa kwanza kutoka kushoto) akizungumza na Mwekezaji wa kiwanda cha kukamua mafuta kwenye maganda ya korosho Bw. Youngwoong Kim, kiwanda hicho kinajengwa Mkuranga Mkoani Pwani.

# CAMARTEC Fast Tractor (CFT-222)

**Uwezo: Inapanda ekari 10-15 kwa siku, Inaweza kupanda mistari 4-6 kulingana na aina ya zao**

**Vipimo: 1980mm x 1900mm x 1630mm;**
**Uzito: Kilo 200-250;**

**Inavutwa kwa trekta yenye uwezo wa 22HP na kuendelea;**

**Bei: Sh. 4,000,000; na**
**Faida inaweza kuanza kupatikana ndani ya miaka miwili (2)**




**CAMARTEC Arusha:**
+255 739 515 254/+255 272 549 000 dg@camartec.go.tz



Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikali
Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara
S.L.P 2996, 40478 Dodoma, Tanzania Mji
wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Viwanda
Simu: +255 26 2963470
Nukushi: +255 26 2963117
Barua pepe: ps@mit.go.tz gcu@mit.go.tz